

Kiowevu cha Silver Diamine Fluoride (SDF) ni nini?

SDF ni kioevu kinachoweza kupakwa kwenye meno ili kuzuia kuoza kwa meno. SDF hupakwa kwenye meno bila kutumia sindano au kitoboa shimo, kwa hivyo inaweza kuwa na manufaa hasa kwa wakaaji wa Vermont ambao wanatatizika kupata huduma ya afya ya meno. Matibabu ya kuoza kwa meno kwa kutumia SDF huenda yasisuie hitaji la kujaza jino lililoathiriwa mara kwa mara katika siku zijazo.

Ni utaratibu gani utatumika kupaka SDF katika meno ya mtoto wangu?

- Mtaalamu wa usafi wa meno atakausha meno ya mtoto wako.
- Atapaka SDF kwenye vijishimo kwa kiasi kidogo sana na kuiruhusu ikauke kwa dakika moja.
- Fahamu kwamba SDF itageuza rangi ya kijishimo kuwa nyeusi. Angalia picha hapa chini.
- Mtoto wako anaweza kuhisi ladha ya metali mdomoni mwake, lakini itaisha haraka.
- Ikiwa SDF itagusana na ngozi na/au ufizi, itasababisha madoa ya muda mfupi.
- Ikiwa SDF itapakwa kwenye jino ambalo lina mjazo wenye rangi ya jino, inaweza kusababisha madoa.

Tafadhali mjulishe mtaalamu wa usafi wa meno ikiwa mtoto wako ana matatizo yoyote kati ya yafuatayo:

- Mzio wa madini ya fedha au metali nyingine
- Vidonda vya mdomo vyenye maumivu
- Mwasho wowote usio wa kawaida kwenye ngozi baada ya kutumia bidhaa fulani

Baada ya utaratibu huu:

- Mtoto wako hapaswi kupiga mswaki kwa muda uliosalia kwa siku hiyo.
- Athari zilizo rodheshwa hapo juu hazijumuishi athari zote zilizo ripotiwa na mtengenezaji wa dawa. Ikiwa utaona athari nyingine ambazo hazija rodheshwa hapo juu, tafadhali wasiliana na muuguzi wako wa shule.
- Ikiwa mtoto wako hana daktari wa meno wa kawaida, mtaalamu wa usafi wa meno atakusaidia kupata mahali ambapo mtoto wako anaweza kupata huduma endelevu ya meno na ya kina.
- Matibabu ya SDF yanapaswa kurudiwa ndani ya miezi sita ijayo ikiwa mtoto wako bado hajapata matibabu ya meno.

Meno ambayo yametibiwa kwa kutumia SDF:



Photo Credit: Dr Jeanette MacLean



Photo Credit: Dr Jeanette MacLean

Mimi, _____, nimesoma fomu hii na kuelewa matibabu. Nimeelezwa kuhusu matibabu, ikiwa ni pamoja na hatari na faida, na nimeridhika na nimepata nafasi ya kuuliza maswali. Ninaelewa kuwa hakuna ahadi kwamba matibabu haya yatakuwa na mafanikio. Ninaidhinisha mtaalamu wa usafi wa meno mwenye leseni kufanya utaratibu huu.

Tarehe: _____ Saini ya Mgonjwa: _____

Saini ya Mzazi, Mlezi au Mwakilishi wa Kisheria wa Mgonjwa (ikiwa anahusika): _____

Saini ya shahidi: _____

Ruhusa hii ni halali hadi itakapobatilishwa na mzazi au mlezi wa kisheria wa mtoto.